KKKT | KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA

# TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

**Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT)** ilizaliwa rasmi mnamo tarehe 19 Juni 1963 ambapo Makao Makuu yapo Arusha. Utume wa KKKT ni kutoa huduma jumuishi kwa watu wote. Usimamizi na uongozi wa Kanisa unatekelezwa na Katibu Mkuu wa KKKT akisaidiwa na Manaibu Katibu Mkuu wanne - wakiwemo Naibu Katibu Mkuu Misioni na Uinjilisti, Naibu Katibu Mkuu Huduma za Jamii na Kazi za Wanawake, Naibu Katibu Mkuu Mipango na Maendeleo na Naibu Katibu Mkuu Fedha na Utawala.
KKKT inakusudia kuajiri mtu mwenye sifa, kujituma na uwezo mkubwa katika nafasi iliyoelezwa hapa chini. Waombaji wote wanashauriwa kusoma na kuzingatia maelekezo na mwongozo wa maombi ya kazi husika.

**Nafasi: NAIBU KATIBU MKUU – MISIONI NA UINJILISTI (Nafasi 1)**
**Anaripoti kwa**: Katibu Mkuu wa KKKT
**Kituo cha kazi**: Makao Makuu ya KKKT (kwa sasa ni Arusha) na kusafiri mara kwa mara ndani na nje ya nchi.
**Muda wa Mkataba**: Miaka mitano, na upo uwezekano wa kuongezewa mkataba mwingine mmoja endapo utendaji wa kazi utaridhisha.

**Muhtasari wa Nafasi**
Naibu Katibu Mkuu – Misioni na Uinjilisti atasimamia, kupanga na kuratibu shughuli zote za Idara ya Misioni na Uinjilisti ikiwa ni pamoja na: Kutengeneza Mkakati wa Misioni, Kuanzisha Makanisa na Ukuaji wake, Uinjilisti na Kushirikisha Imani, Usimamizi wa Maandiko ya Kanisa na kuhakikisha Misingi ya Imani inazingatiwa, Ushirikiano na Mitandao ya Misioni ya ndani na nje ya nchi, pamoja na shughuli za Elimu ya Kikristo na kuendeleza Makanisa yaliyopo.

**Majukumu ya Kawaida na ya Jumla**

1. **Uongozi na Usimamizi**
   Kutoa uongozi na usimamizi wa jumla kwa shughuli zote zinazohusu Misioni na Uinjilisti ndani na nje ya Kanisa.
2. **Mpango Mkakati na Uratibu**
   Kupanga, kuratibu, kuongoza na kufuatilia mikakati ya Kanisa katika kutangaza Injili ndani na nje ya Tanzania.
3. **Uratibu wa programu za Kichungaji**
   Kusimamia na kuunganisha mipango ya kichungaji hasa katika elimu ya Kikristo, utetezi, ushirikishwaji wa vijana na usambazaji wa maandiko matakatifu.

4. **Uendelezaji wa Mitaala**
   Kushiriki katika utayarishaji na tathmini ya mitaala ya elimu ya theolojia na ya Kikristo katika taasisi na vituo vya mafunzo vya Kanisa.
5. **Upanuzi wa Misioni**
   Kuratibu uanzishwaji na uendelezaji wa maeneo ya misioni kwa lengo la kueneza imani ya Kilutheri kitaifa na kimataifa.
6. **Vituo vya Misioni na Mawasiliano**
   Kusimamia shughuli za vituo vya misioni na miradi ya kuinua uinjilisti, ukuaji wa kiroho na mawasiliano.
7. **Uongozi wa Kiroho Makao Makuu ya KKKT**
   Kuhudumu kama *Chaplain* wa Makao Makuu ya Kanisa na kuandaa program za kiroho za kuimarisha watumishi na wachungaji waliopo.
8. **Uratibu wa Mikutano ya Maaskofu na Mafunzo**
   Kusimamia maandalizi na utekelezaji wa mikutano ya Maaskofu na shughuli za pamoja.
9. **Uwasilishaji wa Taarifa na Uwajibikaji**
   Kuwasilisha taarifa kwa Katibu Mkuu wa KKKT na kuhakikisha shughuli zote zinaendana na Maono na Utume wa Kanisa.
10. **Mkutano wa Wachungaji wa KKKT**
    Kupanga na kuratibu Mkutano wa Wachungaji wote wa KKKT kila baada ya miaka minne na kuhakikisha matokeo ya mkutano yanasambazwa kwa dayosisi zote.

**Sifa, Uzoefu na Ujuzi Unaohitajika:**

1. Awe Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT).
2. Awe na mwenendo mzuri wenye ushuhuda na kuhudumu kwa namna inayodhihirisha maadili na matarajio ya KKKT.
3. Awe na Shahada ya *Divinity*/Theolojia.
4. Shahada ya Uzamili itakuwa ni sifa ya ziada.
5. Awe na uzoefu wa zaidi ya miaka mitano (5) katika uongozi wa shughuli za Misioni na Uinjilisti.
6. Awe na uzoefu wa kusimamia na kuendeleza mipango ya ukuaji wa Kanisa.
7. Awe na ujuzi wa kuwasiliana na kushirikiana na watu wa makundi mbalimbali.
8. Awe na uongozi madhubuti, ujuzi wa kusimamia watu na rasilimali, na mawasiliano bora.
9. Awe mwaminifu kwa dhamira ya KKKT, awe na uwezo wa kushirikiana na watu mbalimbali, na kuwa na uwezo wa kuchanganua changamoto na kutatua matatizo.
10. Awe mwanachama hai wa KKKT na mwaminifu katika kutimiza maono na utume wa KKKT.
11. Awe na umri kati ya miaka 40 hadi 55, akiwa mwenye akili timamu na afya njema.
12. Awe na ujuzi wa kompyuta na matumizi ya programu za *Microsoft.*

**Mshahara**

Mshahara utazingatia viwango vya mshahara vya KKKT.

**NAMNA YA KUTUMA MAOMBI:**
Tuma *barua ya maombi, vyeti vya kitaaluma, cheti cha ndoa (kama umeoa/umeolewa),* na wasifu binafsi (*CV*) pamoja na majina ya wadhamini (*referees*) watatu na mawasiliano yao, vyote kwa pamoja vitumwe katika **faili moja la PDF** kabla ya siku ya mwisho ya kupokea maombi.

Barua ya maombi ielekezwe kwa:
**Mwenyekiti**
**Kamati ya kumtafuta Naibu Katibu Mkuu Misioni na Uinjilisti**
**Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania**
**S.L.P 3033**
**ARUSHA**

**MAELEKEZO MUHIMU:**

1. Maombi YOTE lazima yaidhinishwe na Askofu wa Dayosisi au Msaidizi wa Askofu.
2. Maombi YOTE yatumwe kwa **baruapepe** kupitia: ***recruitment@elct.or.tz***
3. Taja nafasi unayoomba kwenye mstari wa kichwa cha baruapepe: *“Application for Deputy Secretary General – Mission and Evangelism position.”*
4. Maombi yote yawe kwenye **faili moja tu la PDF** lenye jina la mwombaji.
5. Kila mwombaji anatakiwa kutuma **maombi mara moja tu.**
6. Waombaji waliochaguliwa tu ndio watakaoitwa kwenye usaili.
7. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **18 Juni 2025.**

**“KKKT ni mwajiri anayezingatia usawa wa fursa kwa wote.”**